

Dhima za Kipragmatiki za Kialami Pragmatiki ‘eh’ katika Kiswahili cha Mazungumzo

Magreth J. Kibiki¹ na Pendo S. Malangwa²

¹Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam (DUCE), Tanzania

²Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Ikisiri

Vialami Pragmatiki (VIPRA) ni eneo ambalo limepata mashiko katika uwanja wa isimu. Hali hii imepelekea VIPRA kuchunguzwa katika lugha mbalimbali ulimwenguni kama vile Kiingereza (Taz. Schiffrin, 1987 na Zarei, 2013), Kijerumani (Taz. Hogeweg na wenzake 2016), Kidachi (Taz. Hoek, 2013), Kigiriki (Taz Archakis, 2001), Kichina (Taz. Chen na He, 2001), Kiitaliano (Taz. Bazanella, 1990), Kihispania (Taz. Durán na Unamuno, 2001) Kituruki (Taz. Yilmaz, 2004) na Kiindonesia (Taz. Nasir, 2017). Hata hivyo, VIPRA katika lugha ya Kiswahili havijachunguzwa. Makala haya yanakusudia kuchunguza kuhusu dhima za kipragmatiki za kialami pragmatiki (KIPRA) *eh* katika Kiswahili cha mazungumzo. Data za makala haya zimekusanywa kutoka katika mazungumzo yasiyo rasmi yanayofanywa na wazungumzaji wa Kiswahili katika maeneo yasiyo rasmi kama vile kwenye vijiwe vya kahawa na vijiwe vya mamantilie. Matokeo ya uchunguzi huu yanaonesha kwamba licha ya KIPRA *eh* kuwa na maana yake ya msingi ambayo ni kukubaliana na jambo, huchanua pia maana nyingine za ziada kama vile mshangao, swali na msisitizo. Tabia hiyo hukifanya KIPRA hicho kuwa na dhima mbalimbali za kipragmatiki.

Maneno Muhimu: Pragmatiki, Kiswahili, Kialami, Mazungumzo

Utangulizi

Hivi karibuni, tafiti kuhusu lugha ya mazungumzo zimeongezeka. Hali hii imesababisha kupewa umuhimu kwa vipashio ambavyo hapo awali vilikuwa vikichukuliwa kuwa havina maana na vilivyorudiwa rudiwa tu bila sababu ya msingi. Hivi sasa, baada ya tafiti mbalimbali kufanyika, vipashio hivi vinachukuliwa kama vipashio muhimu vya kimawasiliano miongoni mwa wazungumzaji (Alami, 2016). Deborah Schiffrin ndiye mwanaisimu wa kwanza kuchunguza kwa kina kuhusu VIPRA katika miaka ya 1980 (Taz. Fraser, 1999,

Yang, 2011 na Alami, 2016). Tangu kugunduliwa kwake, VIPRA vimepata mashiko katika uwanja wa isimu. Hali hii imefanya VIPRA kuchunguzwa katika lugha mbalimbali duniani. Uchunguzi kuhusu VIPRA umefanywa kwa mitazamo na mielekeo tofautitofauti. Baadhi ya wanaisimu wamevichunguza VIPRA kwa kujikita katika mwelekeo wa kisosholojia (Taz. Erman, 1999). Lengo hasa ni kuonesha namna VIPRA vinavyotumiwa na wazungumzaji kwa kuzingatia jinsi na umri. Wengine wamevichunguza wakijikita katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha (Taz. Yang, 2011 na Li, 2015). Pia, wengine wamejikita katika kuchunguza namna VIPRA vinavyofanya kazi katika matini wakijielekeza zaidi kuonesha namna VIPRA vinavyojenga ushikamani katika matini (Taz. Schiffirin, 1987; Redeker, 1991 na Lenk, 1998). Halikadhalika, wengine wamechunguza VIPRA wakivihusisha na taaluma ya tafsiri. Lengo hasa ni kuonesha kuwa VIPRA vina changamoto katika tafsiri (Taz. Stede, 2000). Wanaisimu wengine wamechunguza VIPRA wakijikita katika uwanja wa pragmatiki hasa wakimakinikia katika kuonesha dhima mbalimbali za kipragmatiki za VIPRA (Gold na Tremblay, 2006; Heylen na Truong, 2010; Hoek, 2013 na Nasir, 2017).

Hata hivyo, tafiti zilizofanywa kuhusu dhima za kipragmatiki za VIPRA kama vile Gold na Tremblay (2006), Heylen na Truong (2010), Hoek (2013) na Nasir (2017) zinaonesha kwamba, licha ya kudhihirisha ufanano, dhima za kipragmatiki za VIPRA hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Mambo haya yametuchoea zaidi kuchunguza kuhusu dhima za kipragmatiki za KIPRA *eh* katika Kiswahili cha mazungumzo. Tumeteua KIPRA *eh* kwa sababu uchunguzi wa awali tuliofanya unaonesha kuwa KIPRA hiki hutumiwa sana na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na hivyo kinaweza kuwa na dhima nyingi za kipragmatiki.

Mapitio ya Maandishi

Katika mjadala wa mapitio ya maandiko, tutaangalia istilahi ya VIPRA na fasili yake, sifa na aina mbalimbali za VIPRA, mjadala wa KIPRA *eh* pamoja na mjadala wa nadharia zinazohusu VIPRA na ambazo zimeongoza utatit wetu. Mjadala hasa unalenga kupambanua pengo au upungufu uliopo katika maandiko yaliyotangulia kwa lengo la kuonesha umuhimu wa kufanyika kwa utafiti huu. Aidha, mapitio yanatumika pia kuonesha uhusiano wa utafiti wetu na tafiti zilizotangulia.

Istilahi na Fasili ya VIPRA

Uchungu kuhusu VIPRA ni eneo ambalo limewavutia wanaisimu wengi kwa siku za hivi karibuni. Hata hivyo, bado hakuna istilahi moja inayotumiwa na waanaisimu wote wanapovirejelea. Wataalamu tofautitofauti wanatumia istilahi tofautitofauti kuvirejelea vipashio hivyo. Wapo wanaisimu wanaotumia istilahi hii ya VIPRA (mfano, Fraser, 1996) na wengine wanatumia istilahi ya vialami kilongo (mfano, Schiffirin, 1987). Aidha, wataalamu wengine wanatumia istilahi ya chembechembe kilongo kama vile Gold na Tremblay (2006), wengine wanatumia

istilahi ya viungishi kilongo (mfano, Biq, 1990) na wengine wanatumia istilahi ya matamko ya kipragmatiki (mfano, Erman, 1987). Ukichunguza kwa karibu istilahi hizi utangundua kwamba majina yanayotolewa ni ya kidhima zaidi. Hii ina maana kwamba tofauti hizi za istilahi zinaashiria kuwa VIPRA vina dhima nyingi na vimekuwa vikichunguzwa kwa mitazamo na mielekeo tofautitofauti (Coll, 2010). Katika makala haya tutatumia istilahi ya VIPRA kwa kuzingatia hoja inayotolewa na Aijmer na Simon-Vandenberg (2006) kwamba VIPRA ni dhana pana zaidi. Wanasisitiza kuwa VIPRA vinahusu hasa matumizi ya alama ambazo humsaidia mshiriki wa mazungumzo kufasili maana katika muktadha wa mazungumzo. Pia istilahi hii imeteuliwa kwa sababu inaendana na taaluma tunayoishughulikia ambayo ni pragmatiki.

Changamoto kuhusu VIPRA haiishii katika istilahi tu, bali pia hata katika fasili yake. Mpaka sasa hakuna fasili moja inayotumiwa na wanaisimu wote kuvirejelea vipashio hivyo. Wanaisimu tofautitofauti wamevifasili VIPRA kwa namna tofauti na hapa tutarejelea baadhi tu ya wanaisimu. Tukianza na Schiffrin (1987) anafasili VIPRA (akitumia istilahi ya vialami kilongo) kuwa ni vipashio vya usemaji vinavyofungua au kufunga usemi. Fasili hii ya Schiffrin (1987) inazua utata kwani haiweki bayana vipashio anavyovirejelea. Pia imezingatia zaidi vipashio vinavyowekwa mwanzoni au mwishoni mwa usemi tu (vinavyofunga au kufunga usemi) na kuacha vile vinavyoweza kuwekwa katikati ya usemi. Tofauti na Schiffrin (1987), Redeker (1991) anafasili VIPRA kuwa ni neno au kirai ambacho hutamkwa kwa lengo la kumfanya msikilizaji awe makini juu ya uhusiano baina ya kinachosemwa sasa na kitakachosemwa baadaye (S1 na S2) katika kilongo cha mazungumzo. Fasili hii ya Redeker (1991) imetusaidia kubaini kuwa KIPRA kinaweza kuwa neno au hata kirai na dhima yake ni kuweka uhusiano baina ya sentensi katika kilongo cha mazungumzo. Hata hivyo, fasili yake imemuegemea msikilizaji peke yake ilhali hata msemaji vinamsaidia kuelewa ikiwa mzungumzaji wake anafuatilia kinachosemwa. Naye Fraser (1999), anafasili VIPRA kuwa ni maneno au virai kutoka katika kategoria mbalimbali za kisintaksia kama vile viunganishi, vielezi na virai vihusishi ambavyo huashiria uhusiano baina ya sentensi inayosemwa sasa na ya awali (S2 na S1). Anasisitiza kuwa VIPRA huwa na maana zake za msingi ambazo ni za kimchakato¹ na maana zake za ziada ambazo hutegemea muktadha wa matumizi. Tukichunguza fasili za Redeker (1991) na Fraser (1999), tunaona kwamba Redeker (1991) anakubaliana na Fraser

¹ VIPRA hurejelewa kuwa vina maana za kimchakato kwa sababu havina vijenzi semantiki bayana vinavyotumika kuvifafanua kama ilivyo katika maneno *baba*, *meza* na *kadhali*. Maana zake za msingi hutegemea namna kipashio hicho kinavyosaidia kulifasiri tamko la sasa kwa kuhusianisha na tamko la awali au linalofuatia (Fraser, 1996).

(1999) kuwa VIPRA vinaweza kuwa maneno au virai kutoka katika kategoria mbalimbali za kisintaksia lakini wanatofautiana katika kuelezea suala la uhusiano unaodhihirishwa na VIPRA baina ya sentensi. Wakati Redeker |(1991) anaona VIPRA hudhihirisha uhusiano baina sentensi inayosemwa sasa na itakayosemwa baadaye (S1 na S2), Fraser (1999) yeye anaona VIPRA huonyesha uhusiano baina ya sentensi inayosemwa sasa na iliyosemwa awali (S2 na S1). Utata huu unazongolewa katika fasili ya Van Bergen na Degand (2013) ambao wanafafanua kuwa VIPRA hudhihirisha uhusiano baina ya sentensi inayosemwa sasa na sentensi iliyosemwa/zilizosemwa kabla au baada ya hiyo inayosemwa sasa katika kilongo cha mazungumzo.

Japokuwa fasili ya Redeker |(1991), Fraser (1999) na Van Bergen na Degand (2013) vimetusaidia kuelewa juu ya dhana ya VIPRA, bado haziweki wazi je ni nafasi zipi ambazo VIPRA hukaa katika sentensi. Kwa upande mwingine, Fung na Carter (2007) wanafasili VIPRA kuwa ni vipashio vya kiisimu ambavyo huweza kupachikwa ndani au nje ya sentensi (mwanzoni, katikati au mwishoni mwa sentensi) katika mazungumzo ili kujenga uhusiano baina ya matamko na kudhihirisha ushirikiano katika mazungumzo baina ya mzungumzaji, msikilizaji na ujumbe unaowasilishwa. Anasisitiza kuwa VIPRA huwa ni vya hiari. Hii ina maana kwamba huweza kuondolewa katika muktadha wa sentensi bila kubadili maana ya msingi ya sentensi hiyo na wala kuathiri masharti ukweli ya sentensi husika.

Tofauti na fasili zilizotolewa na Redeker |(1991), Fraser (1999), Van Bergen na Degand (2013), Fung na Carter (2007) wanatumia istilahi ya tamko badala ya sentensi. Hii ina maana kwamba VIPRA havitumiki tu kuashiria uhusiano baina ya sentensi bali huweza kuashiria uhusiano baina ya matamko katika kilongo cha mazungumzo. Tamko katika muktadha huo linaweza kuwa neno, kirai, kishazi, sentensi, aya na kadhalika. Licha ya kutofautiana katika fasili zao, Redeker (1990), Fraser (1999), Fung na Carter (2007) na Van Bergand na Degand (2013), wote wanakubaliana kuwa VIPRA vina dhima nyingi na ni vya aina nyingi. Wanasisitiza kuwa VIPRA huwa na maana zake za msingi lakini huweza kuchanua maana mbalimbali kutegemea na muktadha wa matumizi katika tamko linalohusika.

Kwa kuzingatia maelezo na ufafanuzi wa wataalamu hawa, kwa ujumla tunaweza kusema kwamba VIPRA ni maneno au virai kutoka katika kategoria mbalimbali za kisintaksia, kama vile vielezi, viunganishi, vitenzi, vihisishi na virai vihusishi. Dhima ya maneno au virai hivyo ni kusaidia kumuelewesha mshiriki wa mazungumzo kufasili uhusiano baina ya tamko linalosemwa sasa na linalosemwa kabla au baadaye katika kilongo cha mazungumzo. VIPRA huwa na maana zake za msingi ambazo ni za kimchakato. Maana hizo hutajirishwa na muktadha vinamotumika. VIPRA haviathiri maana ya msingi ya sentensi wala haviathiri masharti ukweli ya sentensi inayohusika. Aidha, VIPRA huweza kuondolewa

katika sentensi bila kuathiri maana ya msingi ya sentensi inayohusika. VIPRA huweza kujitokeza mwanzoni, mwishoni na hata katikati ya sentensi.

Mapitio kuhusu Sifa na Aina Mbalimbali za VIPRA

VIPRA huwa na sifa mbalimbali zinazovitambulisha. Tutajadili baadhi ya sifa hizo kama zinavyofafanuliwa na O'Neal (2013). Kwa kuanza na sifa za kisemantiki, O'Neal (2013) anafafanua kuwa VIPRA vina sifa ya kuchanuza maana za msingi kwa kiasi kidogo au havina maana hiyo ya msingi kabisa. Pia kuwepo kwa KIPRA au kuondolewa kwake katika tamko hakuna athari kwenye maana ya msingi ya tamko linalohusika. Sifa nyingine ni kuwa VIPRA vina sifa ya upolisemia, hasa kutokana na maana zake za ziada. Hii ina maana kwamba licha ya VIPRA kuwa na maana zake za msingi, huchanuza maana nyingine za ziada. Pia, VIPRA vina sifa ya kupauka au kuchakaa kisemantiki. Hii ni kwa sababu maana za msingi za VIPRA huwa zinachakaa au hazitumiki sana ikilinganishwa na maana za kipragmatiki. Hivyo, huifanya maana hiyo ya msingi kupauka au kuchakaa na hatimaye, kupotea kabisa. Kipragmatiki, VIPRA huhusishwa na muktadha wa usemaji. Hii ina maana kwamba maana za VIPRA hutegemea nini kimesemwa kabla au baada ya hicho kinachosemwa sasa katika kilongo cha mazungumzo. Maana hizo pia hutegemea dhamira ya mzungumzaji kuhusu kile anachotaka msikilizaji akitafsiri zaidi ya maana ya msingi ya tamko linalohusika. Kisintaksia, VIPRA huweza kujitokeza mwanzoni, katikati au mwishoni mwa sentensi na ni vya hiari yaani vinaweza kutumika au visitumike na kuondolewa kwake hakuathiri maana. Pia, VIPRA haviathiriki na uhamishaji wa vipashio vya kisintaksia kwenye tungo na huweza kufanya kazi katika ngazi zaidi ya sentensi. Aidha, muktadha au nafasi ambamo VIPRA vinakaa ni muhimu katika kuashiria maana ya VIPRA hivyo. Ingawa O'Neal (2013) amtusaidia kuelewa sifa mbalimbali za VIPRA, anaeleza sifa hizo kwa kujikita katika lugha ya Kiingereza. Hivyo basi, kuna haja ya kuchunguza VIPRA katika lugha ya Kiswahili na kubaini namna vinavyojidhihirisha katika lugha hiyo.

Ni vyema tukibainisha hapa aina mbalimbali za VIPRA kabla hatujajadili hicho kimoja. Wataalamu mbalimbali kama vile Fraser (1999), Schiffirin (2001), Coll (2010) na Zarei (2013) wanakubaliana kwamba VIPRA katika lugha ni vingi na ni vya aina nyingi. Coll, (2010) kwa mfano anadokeza kuwa KIPRA kinaweza kuwa neno au hata kirai. Kwa upande mwingine, Zarei (2013) anafafanua kuwa VIPRA huhusishwa na kategoria za kisintaksia kama vile vielezi (mfano; *sasa (now)*, *kwa hakika (actually)* na *labda (anyway)*), viunganishi viambatizi na viunganishi vitegemezaji (mfano; *na (and)*, *lakini (but)*, *kwa sababu (because)*), vihisishi (kama vile; *oh!* na *gosh!*), Vitenzi (mfano; *sema/niambie (say)*, *angalia/tazama (look)*) na vishazi (kama vile; *unaona (you see)*, *ninamaanisha (I mean)* na unajua (*you know*). Hata hivyo, aina na mifano ya VIPRA inayoelezwa na wataalamu hawa inahusu hasa lugha ya Kiingereza na si lugha ya Kiswahili. Hivyo

basi, tafiti zaidi zinahitajika ili kuchunguza VIPRA katika lugha ya Kiswahili na hilo ndio lengo la makala haya.

Mapitio ya Maandiko kuhusu KIPRA *eh* katika Lugha Mbalimbali

Tafiti mbambali zimefanywa kuhusu KIPRA *eh*. Wataalamu kama vile Avis (1972), Johnson (1972) na Gold na Tremblay (2006) wamefanya tafiti kuhusu KIPRA *eh* katika lugha ya Kiingereza kinachozungumzwa Kanada. Avis (1972) alifanya utafiti mdogo ambao lengo lake ni kupata maoni ya wazungumzaji wa Kiingereza kama wanatumia KIPRA *eh* katika sentensi kuashiria dhima ya kipragmatiki ya *kiangami swali* na *kumtaka mzungumzaji arudie alichosema*. Katika utafiti wake anaonyesha kuwa matumizi ya KIPRA *eh* kuashiria dhima ya *kiangami swali* ndiyo yalionekana kukubalika zaidi ikilinganisha na yale ya *kumtaka mzungumzaji arudie alichokisema*. Hata hivyo utafiti huu ulishughulikia dhima mbili tu zinazotokana na KIPRA *eh*. Aidha mtafiti alitumia mbinu ya hojaji kupata data. Tofauti na Avis (1972) makala haya yamejikita katika kuchunguza dhima za kipragmatiki za KIPRA *eh* kama kinavyotumiwa na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Pia, data zilizotumika zimepatikana kwa kutumia mbinu ya ushuhudiani-ushiriki na si hojaji, hivyo tunaamini utafiti huu ni wa kina na umetupatia matokeo yanayochangamsha zaidi na yanayosogeza mbele utafiti wa VIPRA katika lugha mbalimbali.

Johnson (1972) tofauti na Avis (1972) anachunguza maana mbalimbali zinazochanuzwa na KIPRA *eh* akiongozwa na nadharia ya tendo uneni ya Austin (1962) katika kuchambua data za utafiti wake. Katika utafiti wake alibaini kuwa kwa kutumia KIPRA *eh* katika sentensi, mzungumzaji anakuwa ametenda matendo uneni kama vile *kutoa maoni, maelezo, maswali, amri, kebehi* na *lawama*. Utafiti wa Johnson (1972) umetusaidia kubaini kwamba KIPRA *eh* kina chanuza maana tofautitofauti za kipragmatiki katika mazungumzo. Hata hivyo, bado anatumia mbinu ya hojaji kupata data za utafiti wake kama ilivyo kwa Avis (1972). Tofauti na Johnson (1972) makala haya yanaongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Mazungumzo kama itakavyofafanuliwa hapo baadaye.

Tofauti na Avis (1972) na Johnson (1972), wanaisimu kama vile Gold na Tremblay (2006) wanafanya ulinganishi wa KIPRA *eh* katika Kiingereza cha Kanada na KIPRA *eh* (*hein*) katika lugha ya Kifaransa. Wanatumia mbinu ya hojaji kubaini maana na mitazamo ya wazungumzaji juu ya VIPRA hivyo. Utafiti wa Gold na Tremblay (2006) unaonesha kuwa licha ya KIPRA *eh* kuwa na dhima za kipragmatiki zinazofanana katika lugha hizo, kuna tofauti pia katika dhima hizo. Kwa mfano, wakati KIPRA *eh* kina dhima ya kipragmatiki ambayo ni kuashiria *swali* katika Kiingereza cha Kanada, dhima hiyo haijitokezi katika Kifaransa. Pia, wakati KIPRA *eh* (*hein*) katika Kifaransa kina dhima ya kipragmatiki ambayo ni *a kushitukiza*, dhima hiyo haijitokezi katika Kiingereza cha Kanada. Kwa ujumla, utafiti wao umetusaidia kuelewa kwamba KIPRA *eh* kina dhima mbalimbali za

kipragmatiki na dhima hizo zinatofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Utafiti kama wa Gold na Tremblay (2006) ulituchoea zaidi kufanya utafiti huu wa KIPRA *eh* katika lugha ya Kiswahili kwani umetuonesha kwamba kuna uwezekano wa kuja na majibu tofauti. Hata hivyo, Gold na Tremblay (2006) wanakiri kwamba mbinu ya hojaji si mbinu nzuri za kupata data kuhusu VIPRA. Hii ni kwa sababu wazungumzaji huwa hawapo makini na hawana hakika kama wanavitumia VIPRA kuchanua maana mbalimbali. Kwa hiyo, tumetumia mbinu ya ushuhudiaji-ushiriki ambayo imetuwezesha kupata data asilia na matokeo kuwa mapana zaidi.

Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Mazungumzo. Mwasisi wa Nadharia ya Usasanyuzi Mazungumzo ni Harvey Sacks miaka ya 1960 (Sacks na Wenzake, 1992). Mawazo ya Sacks yameendelezwa na kuboreshwa na wanaisimu kama vile Jefferson (1985) na Schegloff (1987, 2001). Hata hivyo, makala haya yamejikita zaidi katika misingi ya Nadharia ya Usasanyuzi Mazungumzo kwa mujibu wa Sacks kwa sababu misingi aliyoieleza ndiyo inayosisitizwa ndani ya makala haya.

Madai makuu ya Nadharia ya Usasanyuzi Mazungumzo ni kuwa mazungumzo ni kitendo cha ushirika ambacho mzungumzaji na msikilizaji wanapewa umuhimu sawa katika kufanikisha maana ya kinachosemwa. Mzungumzaji hulipangilia tamko linalowasilishwa kwa msikilizaji na msikilizaji huliitikia tamko lililotelewa na mzungumzaji kwa kutoa mrejesho. Kwa mujibu wa nadharia hii, maana ya umbo lolote la kiisimu huafikiwa ndani ya mchakato wa mazungumzo yenyewe. Hii ina maana kwamba maana haitokani na umbo la kiisimu pekee, bali hutegemea namna washiriki wa mazungumzo wanavyolitumia umbo hilo la kiisimu katika mazungumzo. Nadharia hii inasisitiza pia kuwa maana ya neno si tuami bali huweza kurekebishwa na kuafikiwa na washiriki wa mazungumzo. Hivyo, maana hutegemea ushahidi unaopatikana ndani ya mazungumzo yenyewe kwa kuhusisha na nini kimesemwa kabla na baada ya hicho kinachosemwa sasa.

Nadharia tete ya utafiti huu ni kwamba dhima mbalimbali za kipragmatiki za KIPRA *eh* zinaonekana kukitwa zaidi katika muktadha wa mazungumzo. Hii ina maana kwamba maana za KIPRA hicho hutegemea nini kimesemwa na washiriki wa mazungumzo kabla au baada ya hicho kinachosemwa sasa. Kwa hiyo, tutaona katika mjadala wa matokeo ya utafiti huu dhima mbalimbali za kipragmatiki za KIPRA *eh* katika Kiswahili cha mazungumzo kwa kuzingatia ushahidi unaopatikana ndani ya mazungumzo ya Kiswahili na katika muktadha halisi.

Mbinu

Data za makala haya zilikusanywa kutoka katika mazungumzo yasiyo rasmi yanayofanywa na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili katika vijiwe vya kahawa na vya mamantilie. Vijiwe vya kahawa viliteuliwa kwa sababu, unywaji wa kahawa

huambatana na mazungumzo na hivyo, VIPRA hutumika zaidi. Eneo la utafiti lililotumika kupata data ya utafiti huu ni mkoa wa Dar es Salaam. Mkoa huu uliteuliwa kwa sababu ya urahisi wa kupata vijiwe vya kahawa na vya mamantilie ambavyo ni muhimu kwa utafiti huu. Katika mkoa huu, data zilikusanywa katika wilaya ya Ubungo kata ya Manzese. Kata hiyo ilituuliwa kwa sababu aina zote mbili za vijiwe vilivyotumika kupata data vilipatikana kwa urahisi na hivyo kurahisisha mchakato mzima wa kupata data.

Kwa kuwa mara nyingi vijiwe vya kahawa huwa na wahasika wanaume, ili kupata data inayoakisi matumizi ya VIPRA katika jinsia zote, mazungumzo yanayofanyika katika vijiwe vya mamantilie yalitumika. Aidha, vijiwe vya mamantilie² viliteuliwa kwa sababu mara nyingi shughuli zao huambatana na mazungumzo mchanganyiko na yasiyo rasmi. Wanawake husimuliana na kujadili mambo mbalimbali yanayogusa maisha yao na jamii kwa ujumla. Kwa hiyo, tuliona kwamba katika maeneo haya ni rahisi kupata data kuhusu KIPRA *eh*.

Jumla ya vijiwe 10 vilitumika kupata data ya utafiti huu. Idadi hii ilituuliwa kwa sababu ilituwezeshwa kupata data toshelevu zilizokidhi malengo ya makala haya. Pia, kijiwe kimoja kiliweza kurudiwa zaidi ya mara moja ili kuweza kupata data za kutosha. Vijiwe 10 vilivyotumika vilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji tajwa. Mtafiti aliwatumia wenyeji wa maeneo husika kubainisha vijiwe vya kahawa na vya mamantilie vinavyopatikana katika maeneo yaliyoteuliwa. Ili kuweza kupata data kutoka katika vijiwe hivyo, mbinu ya ushuhudiaji-ushiriki ilitumika. Ushuhudiaji -ushiriki ni mbinu ya kukusanya data ambayo humwezesha mtafiti kupata data kuhusu shughuli mbalimbali za jamii katika mazingira asilia kwa kushuhudia moja kwa moja na kushiriki katika shughuli hizo (Kawulich, 2006).

Mbinu ya ushuhudiaji –ushiriki ilituuliwa kwa sababu ilirahisisha shughuli nzima ya kurekodi mazungumzo kutoka katika vijiwe. Kwa kutumia mbinu hii ya ushuhudiaji-ushiriki, mtafiti alishuhudia moja kwa moja namna mazungumzo yanavyofanyika katika vijiwe hivyo huku akishiriki katika mazungumzo hayo na

² Vijiwe vya mamantilie vilivyotumiwa katika makala haya ni vile ambavyo wanawake huendesha biashara ya kupika chakula. Biashara hiyo hufanyika katika maeneo ya wazi kama vile sokoni, pembezoni mwa barabara na maeneo yenye shughuli za ujenzi. Katika maeneo hayo, mamantilie zaidi ya mmoja hujipanga pamoja na kuendesha biashara hiyo. Mazungumzo ya mamantilie yaliyotumika katika makala haya ni yale yanayowahusu mamantilie wakiwa katika shughuli ya kuandaa chakula na yale ambayo mamantilie huyafanya na wasaidizi wao wakati wa kuandaa chakula. Pia mazungumzo baina ya mamantilie na wateja yamehusishwa katika makala haya.

watafitiwa. Kupitia mbinu hii, mazungumzo yanayofanyika katika vijiwe vya kahawa na vya mamantilie yaliweza kurekodiwa katika kinasa sauti. Data hiyo imetusaidia kufafanua dhima za kipragmatiki za KIPRA *eh* katika Kiswahili cha mazungumzo na kutoa mahitimisho kuhusu hali ya VIPRA katika lugha ya Kiswahili.

Aidha, data zimechambuliwa kwa kufuata mkabala wa kitaamuli. Mkabala wa kitaamuli ni ule ambao data huwasilishwa kwa kutoa maelezo au ufafanuzi kuhusu vipengele mbalimbali muhimu katika utafiti. Enon (1998) anaeleza kuwa, uwasilishaji wa data kwa kutumia mkabala wa kitaamuli ni mchakato binafsi sana ambao hautumii kanuni nyingi za kitakwimu. Hivyo katika makala haya, dhimba mbalimbali za kipragmatiki za KIPRA *eh* zimebainishwa kwa kutoa maelezo na ufafanuzi wa kina kuhusu dhima hizo. Uchambuzi huo umefanyika kwa kufutata hatua zifuatazo: kwanza kabisa, mtafiti alisikiliza kwa umakini kwa kurudia mara kwa mara mazungumzo yaliyorekodiwa katika kinasasauti ili kuteua mazungumzo ambayo yana data anayoikusudia. Hatua hiyo ilifuatiwa na mchakato wa unukuzi wa mazungumzo hayo. Unukuzi wa mazungumzo umefanywa kwa kutumia mfumo wa unukuzi wa Jeffersonian (*Jeffersonian Transcription System*) kama unavyoelezwa na Psathas na Anderson (1993) na kama unavyoonekana katika kiambatisho cha makala haya. Mfumo huu umeteuliwa kwa sababu ni mfumo wa unukuzi unaosisitiza kuzingatia kila kipengele katika mazungumzo ili kuleta athari sawa kwa msomaji. Baada ya kufanya unukuzi, mtafiti alichanganua data akiongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Mazungumzo.

Dhima mbalimbali za Kipragmatiki za KIPRA *eh* katika Kiswahili cha Mazungumzo

Kwa mujibu wa data zilizokusanywa kutokana na mazungumzo yaliyofanywa katika vijiwe vya mamantilie na vijiwe vya kahawa, KIPRA *eh* kilionenakana kuwa na dhima za kipragmatiki kama ifuatavyo;

KIPRA *eh* huweza kutumika katika mazungumzo kuashiria dhima ya kipragmatiki ambayo *ni kiitikio*. Hii ina maana kwamba mzungumzaji huweza kutumia KIPRA *eh* kama ishara ya kuitika kama ilivyo kwa maneno mengine ya Kiswahili kama *abee* na *naam*. Dhima hiyo inajitokeza katika data ifuatayo kutoka katika mazungumzo ya mamantilie na msaidizi wake wa kazi:

Data 1:

1. A. Mama (anaita kwa kutaja jina)
2. B. E::h.
3. A. Mteja amesema anaomba chenji.
4. B. E::h?
5. A. Mteja amesema anaomba CHENJI.
6. B. Shilingi ngapi?

7. A. Mia tano.
8. B. ((anafungua mkoba, anatoa chenji na kumpa)).

Katika data hiyo, mzungumzaji A anaonekana kumwita mzungumzaji B na mzungumzaji B anaitika kwa kutumia KIPRA *eh*. Baada ya kuitika mzungumzaji A anaendelea kuzungumza kile alichokikusudia (anatoa taarifa kuhusu chenji ya mteja). Hivyo ni wazi kuwa katika muktadha huu, KIPRA *eh* kina dhima ya kipragmatiki ya *kiiitiko*. Katika data hiyo, inajitokeza pia dhima nyingine ya kipragmatiki ya KIPRA *eh* ambayo ni *kumtaka mzungumzaji arudie alichosema awali* (sawa na kusema *umesema nini vile?*). Dhima hiyo inajitokeza zaidi katika mazingira ambayo ama msikilizaji hajasikia kabisa kilichosemwa awali au amesikia kwa kiasi na hivyo anataka kupata uhakika kama alichokisikia ni sahihi au la. Katika data hiyo, baada ya mzungumzaji A kumwita mzungumzaji B na kisha mzungumzaji B kuitika, anampa taarifa kuwa mteja anahitaji chenji. Mzungumzaji B anatumia KIPRA *eh* kuashiria kuwa msemaji arudie alichokisema. Ushahidi kwamba KIPRA *eh* kina dhima hiyo unatokana na kitendo cha mzungumzaji A kurudia kile alichokisema awali. Aidha, inadhibitika zaidi katika mstari wa 6 na wa 8 ambapo mzungumzaji B anaonyesha kuwa sasa amesikia vyema na ameelewa na anachotaka kujua ni kiasi gani. Hata hivyo, imedhihirika kwamba KIPRA *eh* kilipotumika kubeba dhima ya *kiiitiko* kilisemwa kwa kutumia kiimbo cha juu (kuashiria swali) huku irabu e ikisemwa kwa kuivuta. Hali hii inaoneshwa kuwa usemaji tofauti wa KIPRA *eh* pia umesaidia kubaini dhima iliyokusudiwa na mzungumzaji katika data hii.

Imeonekana pia kwamba, dhima nyingine ya kipragmatiki inayobebwa na KIPRA *eh* ni *kuweka msisitizo au mkazo katika jambo linalosemwa*. Hapa mzungumzaji anatumia KIPRA *eh* kusesitiza au kuweka mkazo juu ya kile anachosema. Mfano wa data kutoka katika mazungumzo ya vijiwe vya kahawa inadhihirisha dhima hii.

Data 2:

9. A.Aise! hivi ((anataja jina)) utakaa na deni langu mpaka lini?
10. B. Nitakulipa bwana:: si unajua tena ule mpango ulikwama?
11. A. Umeanza habari zako ((akiongea kwa hasira))
12. B. Sio hivyo bwana, kweli siwezi kukudhulumu tumetoka mbali mkuu.
13. A. Agh! ((amekasirika zaidi)) unajua wewe sio kwamba huna hela, *e:h?* = wewe unahela, *e:h?* =Sema tu hujaona kama deni langu ni MUHIMU kuliko mambo yako, *e:h?* = Haiwezekani ukae tu kimya na deni langu mpaka leo hii, *e:h?* unafikiri mimi naishije? ((Anapandwa na hasira ananyanyuka na kumkaba koo mdaiwa)). (0.5) Haya, leo niambie hapa mbele ya hawa mashahidi (anaonyesha kwa mkono mmoja washiriki wengine wawili wa kijiwe). Unalipa::? hulipi? =

14. B. =Nalipa [mkuu.]
15. C. [Jamani, acheni hayo mambo yenu]
16. A. Lini? =
17. B. =Jumatatu=
18. A. =Utalipa jumatatu e::h? =
19. B=Eh mkuu ((huku akitikisa kichwa kama ishara ya kukubaliana))
20. (0.05)
21. A. Sawa, jumatatu usionekane tena UTANITAMBUA.

Katika kilongo hiki cha mazungumzo, mzungumzaji A anaonekana kutofurahishwa na kitendo cha mwenzake kutomlipa deni lake na hivyo katika mstari wa 13 anatumia KIPRA *eh* kutaka kuisitiza kile anachokisema. Mzungumzaji huyo anatumia KIPRA *eh* kwa kukirudia mara kadhaa huku akiongea kwa mfululizo jambo linaloashiria kwamba anaweka msisitizo zaidi juu ya kile anachokisema. Katika kufanikisha dhima hiyo, KIPRA *eh* kinaonekana kusemwa kwa kuweka mkazo katika irabu /e/ na muendelezo kidogo wa irabu hiyo kisha kufuatiwa na kiimbo cha swali katika konsonanti /h/ yenye msikiko hafifu.

Dhima nyingine ya kipragmatiki inayojitokeza katika kilongo cha mazungumzo ya hapo juu (data 2) ni KIPRA *eh* kufanya kazi kama *kiangami swali*. Hapa mzungumzaji A anatumia KIPRA *eh* kumtaka mzungumzaji B kuthibitisha kile anachokisema (sawa na kusema si ndivyo?, siyo? au sawa?). Dhima hiyo inajitokeza katika mstari wa 18 pale mzungumzaji A anaposema =Utalipa jumatatu e::h? = Jibu la mzungumzaji B ambalo linathibitisha kuwa atalipa siku hiyo linaashiria kwamba KIPRA hicho kimebeba dhima hiyo ya *kiangami swali*. Pia, ni vyema kudokeza kwamba utamkaji wa KIPRA *eh* kuashiria dhima hiyo umehusisha uendelezi wa irabu e na kiimbo cha kupanda kinachoashiria swali. Katika data hii pia, KIPRA *eh* kinaonekana kubeba dhima ya kipragmatiki ambayo ni *jibu la swali linalotumika kuashiria kukubaliana na kinachosemwa*. Hapa mzungumzaji B anatumia KIPRA *eh* kuashiria kuwa ameelewa kilichozungumzwa na mzungumzaji A na hivyo anakubaliana na kuthibitisha kwamba atalipa siku hiyo. Dhima hii inajitokeza katika mstari wa 19 ambapo mzungumzaji B anatumia KIPRA *eh* kuashiria kwamba anakubaliana kwamba atalipa. Ushahidi wa kimuktadha unatokana na kitendo cha mzungumzaji A kuridhia jibu hilo kwa kutumia KIPRA *sawa* kuashiria kuridhika au kukubaliana na jibu la mzungumzaji B. KIPRA *eh* katika muktadha huu kinasemwa kwa kiimbo cha kati tofauti na jinsi kilivyotumiwa katika mstari wa 13 na mstari wa 19).

Data iliyopatikana kutoka katika vijiwe vya mamantilie inaonesha kwamba KIPRA *eh* hutumika kama *ishara ya kudumisha mahusiano miongoni mwa wazungumzaji*. Mfano ufuatao baina ya mamantilie na mteja unadhihirisha dhima hiyo:

Data 3:

22. A. Unanidai shi ngapi?
23. B. Alfu mbili tu.
24. A. ((Anatoa pesa na kumpa)
25. B. ((Anapokea)) Asante e::h (°)? = karibu tena e::h (°)?
26. A. Haya asante. ((Anaondoka huku akitabasamu)).

Katika data hii, tunaona kwamba mzungumzaji A anauliza kiasi anachodaiwa na mzungumzaji B anataja kiasi hicho. Baada ya kujua kiasi mzungumzaji A anatoa fedha na mzungumzaji B anapokea na kisha kushukuru. Hapa tunaona kwamba mzungumzaji B anatumia KIPRA *eh* ambacho kinatamkwa kwa kiimbo cha kubembeleza kama ishara ya kudumisha mahusiano baina yake na mteja (Taz. Mstari wa 25). Ingawa KIPRA *eh* kimetamkwa kama kiangami swali, hata hivyo katika muktadha huu hakibebi dhima hiyo. Hii ni kwa sababu hatuoni ushahidi wa mzungumzaji A kujibu na kuthibitisha kilichosemwa. Bali anajibu “Haya asante” na kisha kuondoka. Katika muktadha huu kitendo cha mteja kutabasamu baada ya mzungumzaji B kushukuru na kumkaribisha tena kinaashiria kwamba mteja amefurahia mazungumzo ya mzungumzaji B au ameridhishwa. Hivyo, lengo la mzungumzaji B la kutumia KIPRA *eh* kama ishara ya kudumisha mahusiano linaonekana kujidhihirisha.

Aidha, data kutokana na vijawe vya mamantilie zinaonesha kwamba KIPRA *eh* kinaweza kubeba dhima zaidi ya moja kwa wakati mmoja. KIPRA *eh* kinaweza kufanya kazi kama *kiangami swali*, *kama mbinu ya kunogeshia mazungumzo* na *kama mbinu ya kudumisha mahusiano baina ya wazungumzaji*. Data inayohusu mazungumzo baina ya mamantilie wawili wanaopika eneo moja inathibitisha dhima hizo:

Data 4:

27. A.((Anatoa gauni kutoka katika mkoba na kulikunjua vizuri ili lionekane)) Gauni zuri, e::h (°)?
28. B. E::h (°) zuri sana=umenunua wapi shoga angu, mbona hatuambiani? ((Anasogea, analishika gauni na kuliangalia vizuri))
29. A. Kariakoo ha ha.
30. B. Utanipeleka na mimi jamani e::h (°)?
31. A. Eh(°) , nitakupeleka usijali.

Tukichunguza katika mstari wa 27 na mstari wa 30, wazungumzaji wanaonekana kutumia KIPRA *eh* kama *kiangami swali cha kuomba ridhaa* kwa sababu mara baada ya mzungumzaji A kutumia KIPRA hicho kuashiria dhima hiyo, mzungumzaji B anaonekana kutoa jibu ili kukubali/ kuafiki kile kilichosemwa au kuombwa na mzungumzaji A. Katika mstari wa 27 mzungumzaji A anatumia KIPRA *eh* kama *kiangami swali* akitaka kupata uthibitisho kama gauni alilovaa ni zuri au la? Mzungumzaji B anatumia KIPRA *eh* kama jibu la swali

kuashiria kwamba *anakubaliana na mzungumzaji kwa kuthithibitisha kuwa ni kweli gauni ni zuri*. Baada ya jibu hilo, mzungumzaji A anacheka kidogo kuashiria kuwa amefurahishwa na jibu hilo. Halikadharika, katika mstari wa 30 Mzungumzaji B anatomia KIPRA hicho kama *kiangami swali* akimtaka mzungumzaji A athibitisha kama atampeleka na yeye akanunue gauni hilo au la. Mzungumzaji A anajibu kwa kutumia KIPRA eh na kuthibitisha kwamba atampeleka. Hata hivyo, usemaji wa KIPRA eh katika mstari wa 27 na 30 ni tofauti kidogo. Hapa KIPRA eh kinasemwa kwa kiimbo kinachoashiria upole au kubembeleza jambo ambalo linatuthibitisha kwamba wazungumzaji wanalengo la *kudumisha mahusiano* yao lakini pia kama mbinu ya *kunogeshwa mazungumzo*. Mwingiliano wa dhima pia unajitokeza katika data ifuatayo inayohusu mazungumzo baina ya mamantilie na mwanaye;:

Data 5:

32. A ((Anamwita mtoto kwa kutaja jina))
33. B. Abee!
34. A. Njoo mwanangu we:::
35. B. ((Anajongea alipo mama))
36. A. Dada amekupikia e::h (°)?
37. B. M::h
38. A. Umekula e::h (°)?
39. B. M::h
40. Chakula kitamu e::h (°)?
41. E::h
42. Jamani dada mzuri huyu[[ha ha]]
43. [[ha ha]]....

Katika kilongo hiki cha mazungumzo, Mzungumzaji A anamwita mtoto wake na anaonekana kuongea na mtoto kwa sauti ya kubembeleza. Anatomia KIPRA eh kama *kiangami swali* kutaka kujua kama amepikiwa chakula na dada na amekula au la. Licha ya KIPRA eh kutumika kama *kiangami swali*, katika mistari ya 36, 38 na 40, kinaonekana kubeba dhima nyingine mbili ambazo ni *mbinu ya kunogeshwa mazungumzo* na *mbinu ya kudumisha mahusiano baina ya wazungumzaji*. Usemaji tofauti wa KIPRA eh (hususani matumizi ya kiimbo cha upole au kubembeleza) pamoja na kicheko cha mama na mtoto vinaashiria kwamba licha ya KIPRA eh kutumika kama *kiangami swali bado*, wazungumzaji wanataka *kunogeshwa mazungumzo* na wakati huohuo *kudumisha mahusiano baina yao*. Aidha, matokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba KIPRA eh pia kilionekana kuwa na dhima ya kipragmatiki ambayo ni *mshangao*. Data kutoka katika mazungumzo ya kijiwe cha kahawa inadhihirisha dhima hiyo;

Data 6:

44. A. Unamwona yule mtoto? ((Akionyesha mkono kuelekea kwa binti mrembo anayepita njiani))

45. B. Ha ha ha umeanza mambo yako.
46. C. Binti maashallah (0.5) Mwenyezi Mungu anajua kuumba jamani dah!
47. A, B na C ((Wanacheka kwa pamoja))
48. C. Halafu kama kafanana na binti wa mzee ((Anataja jina))
49. B. E::h, kweli bwana.
50. C. Alishafariki yule binti=
51. B. =E::h! = ((Akionekana kama aliyepigwa na butwaa))
52. A. =Siku nyingi, kwani hujui.
53. B. Sina habari ndugu yangu, dah! masikini!....

Katika kilongo hiki cha mazungumzo, mzungumzaji A anawaonyesha wenzie binti mrembo anayepita njiani. Kitendo hiki kinazua utani au masihara kidogo kisha kufuatiwa na kicheko. Baadaye mzungumzaji B anamfananisha binti huyo na mtoto wa mzee fulani ambaye anaonekana kufahamika na wazungumzaji wengine kisha mzungumzaji C anawafahamisha kwamba binti huyo wanayemzungumzia alishafariki. Taarifa hiyo inaonekana kuwa ngeni kwa mzungumzaji B ambaye anumia KIPRA *eh* kuashiria kushangazwa na taarifa alizozisikia kutoka kwa wazungumzaji wengine (Taz. Mstari wa 51. Hivyo basi, kwa kuzingatia ushahidi huu wa kimuktadha ni wazi kuwa KIPRA *eh* kina dhima hiyo ya *mshangao*.

Dhima nyingine ya kipragmatiki ya KIPRA *eh* ni kutumika kama *kianzilishi cha mazungumzo*. Data kutoka katika mazungumzo ya mamantilie na kutoka katika kijiwe cha kahawa inaashiria dhima hiyo;

Data 7:

54. A. ((Anafika na kuwakuta wafanyakazi wake wakiendelea na kazi))
Eh::, mmeamkaje jamani?
55. B. [[Hatujambo, shikamoo mama]]
56. C. [[Salama, shikamoo]]
57. A. Marhaba, vipi mmeshakoka moto?
58. B. [[Ndiyo]]
59. C. [[Ndiyo]]...

Data ifuatayo kutoka katika kijiwe cha kahawa pia ina nduni hizi:

Data 8:

60. A. ((Anafika na kuwakuta wenzake katika kijiwe)) Eh::, bwana (anataja jina) niambie (huku akimpa mkono ishara ya salamu).
61. B. Ah! = Ninalo basi: (0.3) njaa tu, ha ha.
62. A. ((Huku akiachia mkono na kuelekea kukaa)) Wimbo wa taifa huo, ha ha ha, ((Akimtazama muuza kahawa))Nipe kikombe kimoja bwana mdogo.
63. B. Hawajambo lakini ulikotoka?
64. A. Wazima bwana, Al hamdullillah....

Katika vilongo hivi viwili vya mazungumzo (Taz. Data ya 7 na ya 8), KIPRA *eh* kinaonekana kuwa na dhima ya *kuanzisha mazungumzo*. Wazungumzaji wanaonekana kutumia KIPRA hicho kama njia ya kuanzisha mazungumzo na washiriki wengine wa mazungumzo. Hii ni kwa sababu katika data ya 7 na ya 8 wazungumzaji wanaonekana kufika katika vijijiwe husika na wanaonekana kutumia KIPRA *eh* kabla ya kuzungumza jambo jingine ili kuanzisha mazungumzo na washiriki wengine wa mazungumzo. Aidha, katika muktadha mwingine, KIPRA *eh* kilionekana kuwa na dhima ya kipragmatiki ambayo ni kuashiria kuwa washiriki wengine wa mazungumzo *wapo pamoja na mzungumzaji, wanaelewa kinachosemwa na hivyo wanamtaka mzungumzaji aendelee na anachokisema*. Data kutoka katika kijiwe cha mamantilie (mamantilie mmoja akimsimulia kisa kilichompata mamantilie mwingine) inadhibitisha juu ya dhima hiyo:

Data 9:

65. A. Unajua sio kwamba mimi nimemfukuza=
66. B. =Eh=
67. A. =Ujinga wake ndio umemfanya aondoke=
68. B. =Eh=
69. A. =Mimi nilikuwa namuonya tu kama mwanangu kwamba unavyofanya sio vizuri. Hao wanaume wanakudanganya tu=
70. B. =Eh=
71. A=Na nilidhani amenielewa kwa sababu hapa katikati alikuwa ameacha kabisa hiyo tabia=
72. B =Eh=
73. A=Lakini kumbe anaendelea=
74. B. =Mh! =
75. A. Juzi ndio nimegungua kuwa mjamzito.
76. B. Jamani!
77. A. Sikuwa na jinsi, ilibidi tu jana aondoke.
78. B. Hawa mabinti kwa kweli ni changamoto sana=
79. A. =Yaani ni shida....

Katika kilongo hiki cha mazungumzo, tunaona kwamba mzungumzaji A anamsimulia mzungumzaji B kisa cha msichana wa kazi kuondoka. Mzungumzaji B anaonekana kutumia KIPRA *eh* mara kadhaa (Taz. mstari wa 66, 68, 70 na 72). Kila baada ya mzungumzaji B kutumia KIPRA hicho, mzungumzaji A anaonekana kuendelea kuzungumza zaidi. Hii inadhihirisha kwamba mzungumzaji B anafuatilia na anaelewa kinachosemwa na mzungumzaji A, kwa hiyo anatumia KIPRA *eh* kama ishara ya kumruhusu mzungumzaji A aendelee kuzungumza.

Halikadhalika, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba KIPRA *eh pia hutumika kuuliza swali*. Dhima hii ni tofauti na ile ya *kiangami swali*. Hapa mzungumzaji anatumia KIPRA *eh* kama swali linalohitaji jibu na si kutoa

uthibitisho. Mfano wa data kutoka katika kijiwe cha mamantilie unathibitisha dhima hiyo:

Data 10:

80. A. Jamani nimeweka hela hapa sio muda=nani amechukua?
81. (0.10)
82. A. Nawauliza nimeweka hela hapa NANI amechukua?
83. B. Mi sijachukua atakuwa ((anataja jina) [[huyo::]]
84. C. [[Mwongo mi sijachuchua]]
85. A. Naona ushakuwa mwizi siku hizi ((Huku akimkazia macho mzungumzaji C)).
86. C. Jamani, mi sijaiba.
87. A. Unasema hujaiiba nani ameiba? Eh?
88. B. Sijui mi nilikuwa nahudumia wateja kule....

Katika kilongo hiki cha mazungumzo, inaonekana kuna wizi ambao umetokea. Mzungumzaji A anauliza nani amehusika na wizi huo. Katika mstari wa 4, mzungumzaji B anamtaja mzungumzaji C kuwa amehusika, kitendo hicho kinamfanya mzungumzaji A amuulize zaidi mzungumzaji C. Mzungumzaji C anakataa zaidi, hali inayosababisha mzungumzaji A kuuliza kama yeye hajaiba nani ameiba . Katika mstari wa 87 mzungumzaji A anatumia KIPRA *eh* kama swali. Uthibitisho ni pale mzungumzaji C anapojibu kuwa hafaamu nani ameiba yeye alikuwa anahudumia wateja (Taz. mstari wa 85 na 88).

Kupitia uchunguzi wa vijiwe vya kahawa ilionekana kwamba dhima nyingine ya kipragmatiki ya KIPRA *eh* ni kutumika kuashiria kuwa *mzungumzaji anatafakari, anajaribu kukumbuka jambo au anatafuta cha kusema*. Data kutoka katika kijiwe cha kahawa kimojawapo inadhihirisha dhima hii:

Data 11:

89. A.Hivi lile shamba ulishauza?
90. B. Kitambo sana.
91. A. Ulimuuzia nani? Dah! Nilikuwa nalitamani sana lile shamba lako.
92. B. Yule jamaa (0.5) alikuwa anaitwa:::....eh...eh.. eh...jirani yake na yule bwana (anataja jina).
93. A. Nani? Musa?
94. B. Enhe:, Musa =sawa sawa....

Katika kilongo hiki cha mazungumzo, mzungumzaji A anamwuliza mzungumzaji B kuhusu shamba kama amekwisha liuza au la. Mzungumzaji B anamweleza mzungumzaji A kwamba alishaliuza kitambo. Mzungumzaji A anataka kujua alimuuzia nani na mzungumzaji B anajibu swali hilo lakini anaonekana kusahau jina la aliyemuuzia shamba hilo. Baadaye anakumbuka kuwa

aliyemuuzia shamba ni jirani na bwana (anayemtaja jina). Kitendo hicho kinamfanya mzungumzaji A amtaje jirani huyo na hivyo mzungumzaji B anakumbuka na hapa anatumia KIPRA enhe kama ishara ya kukumbuka jina husika. Kutokana na data yetu hapo juu, ni wazi kuwa KIPRA *eh* kimetumiwa na mzungumzaji B kuashiria kwamba mzungumzaji anatafakari au anajaribu kukumbuka na kutafuta cha kusema (Taz. mstari wa 92).

Dhima nyingine ya KIPRA *eh* ni kuashiria *kughafirika*, *kutokukubaliana* au *kutofautiana* na kinachosemwa. Mfano wa data kutoka katika mazungumzo ya kijawe cha kahawa yanadhahirisha dhima hii;

Data 12:

95. A. ((Anatoa sigara, anaiwasha na kuanza kuivuta))
96. B. Bwana eh, unatumiza na moshi, si utoke hapa ukavutie mbali huko? ((Akionyesha sura ya kukasirika))=
97. C. =Kweli kabisa.
98. A. Mmeshanza mambo yenu, kila mtu ana haki ya kukaa hapa.
99. B. We unataka uambiwe mara ngapi uache kuvuta sigara bwana?
100. A. Eh! (Anaondoka huku akiwa amekasirika)
101. B. Wewe kuwa mbishi tu tutakuzika sio muda...

Katika data hii wazungumzaji wanaonekana kuendelea na mazungumzo na mara mshiriki mmoja wa mazungumzo anaanza kuvuta sigara. Kitendo hicho kinawakera washiriki wengine wa mazungumzo na hivyo kumweleza kuhusu madhara ya kuvuta sigara. Mzungumzaji A anaonekana kutopendezwa na mazungumzo hayo na hivyo anatumia KIPRA *eh* kuashiria kwamba ameghafirika lakini pia hakubaliani au anatafautiana na washiriki wengine wa mazungumzo. Kitendo cha Mzungumzaji Akuondoka mara baada ya kusema KIPRA hicho kinathibitisha zaidi kuhusu dhima hiyo.

Hitimisho

Kutokana na data yetu pamoja na uchambuzi tuliofanya hapo juu, ni wazi kuwa KIPRA *eh* kina dhima mbalimbali za kipragmatiki. Dhima tulizozipata kutokana na utafiti huu ni; kutumika kama *kiititio*, *kumtaka mzungumzaji arudie alichosema awali*, *kuweka msisistizo au mkazo katika jambo linalosemwa*, kutumika kama *kiangami swali*, *kudumisha mahusiano miongoni mwa wazungumzaji*, *kuashiria mshangao*, kutumika kama *kianzilishi cha mazungumzo*, *kuashiria kuwa mzungumzaji anatafakari*, *anajaribu kukumbuka jambo* au *anatafuta cha kusema*, *kuashiria kughafirika*, *kutokukubaliana au kutofautiana na kinachosemwa*. Hata hivyo, ni vyema kuweka bayana kuwa dhima tulizozijadili hapa ni kwa mujibu wa vyanzo viwili tu vya data; ambavyo ni vijawe vya kahawa na vijawe vya mamantilie. Upo uwezekano wa KIPRA *eh* kuwa na dhima nyingine zaidi ya tulizozijadili katika makala haya kama uchunguzi wa kina zaidi utafanyika.

Pia, makala haya yamebaini kwamba kiimbo kina mchango mkubwa katika kubaini dhima za kipragmatiki za KIPRA *eh*. Hii ina maana kwamba usemaji au utamkaji tofauti wa KIPRA *eh* unaonekana unachanuza dhima iliyokusudiwa na mzungumzaji. Hivyo basi, sifa za kiarudhi hususani kiimbo, zinaweza kuchunguzwa zaidi katika utafiti wa dhima za VIPRA. Halikadhalika, makala haya yamebaini kwamba viziada lugha kama vile ishara za viungo vya mwili vina mchango katika kubaini dhima inayobebwa na KIPRA *eh*. Hii ina maana kwamba usemaji wa KIPRA *eh* huambatana na ishara mbalimbali za viungo vya mwili ambazo ni muhimu katika kubaini dhima za kipragmatiki za KIPRA hicho. Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yanadokeza kwamba VIPRA vina dhima mbalimbali katika lugha ya Kiswahili na ni eneo ambalo linadokeza utajiri katika masuala ya utafiti wa kipragmatiki.

Marejeleo

- Aijmer, K. na Simon-Vandenberg, A. (2006) (wah). *Pragmatic Markers in Contrast*. Elsevier Ltd. Netherland.
- Alami, M. (2016). "An Investigation of Pragmatic Functions and Position of Prevalent Persian Discourse Markers Used in Casual Conversation among Tehran Speakers". Katika *International Journal of Applied Linguistics and English Literature*. 5(1):250-263.
- Archakis, A. (2001). "On Discourse Markers: Evidence from Modern Greek". Katika *Journal of Pragmatics*. 33 (8):1235-1261.
- Avis, W.S. (1972). "So eh? is Canadian, eh?". Katika *Journal of Linguistics*. 17:89-104.
- Bazanella, C. (1990). "Phatic connectives as Intonational Cues in Contemporary spoken Italian". Katika *Journal of Pragmatics*. 14 (4) :629-647.
- Biq, Y. (1990). "Conversation, Continuation and Connectives". Katika *Text*. 10 (3):187-208.
- Chen, Y. na He, A.W (2001). "Dui Bu Dui as Pragmatic Markers. Evidence from Chinese Classroom Discourse". Katika *Journal of Pragmatics*. 33:1441-1465.
- Coll, M. U (2010). *The Syntax and Semantics of Discourse Markers*. New York: Continuum International Publishing Group.
- Diskin, C. (2017). "The use of the Discourse-Pragmatic marker 'like' by Native and non-Native speakers of English in Ireland". Katika *Journal of Pragmatics*. 120:144-155.
- Durán, M.E na Unamuno, V. (2001). "The Discourse Marker a ver (Catalan, aveure) in Teacher-Student interaction". Katika *Journal of Pragmatics*. 33:193-208.
- Erman, B. (1987). *Pragmatic Expressions in English: A Study of you know, you see and I mean in Face-to-face conversation*. Stockhorm: Almgvist and Wiksell International.
- _____ (1999). "Pragmatic Markers Revisited with a Focus on 'you know' in Adult and Adolescent Talk". Katika *Journal of Pragmatics*. 33:1337-1359.
- Fraser, B. (1996). "Pragmatic Markers?" Katika *Pragmatics*. 6 (2):167-190.
- _____ (1999). "What are Discourse Markers?" katika *Journal of Pragmatics*. Toleo 31:931-952.
- Fung, L na Carter, R. (2007). "Discourse Markers and Spoken English: Native and Learner Use in Pedagogical Settings". Katika *Applied Linguistics*. 28(3):410-439.

- Gold, E na M. Tremblay. (2006). “Eh? and *Hein?* Discourse Particles or National Icons?” Katika *Canadian Journal of Linguistics*. 51(2/3): 247-264.
- Heylen, D. na Truong, K.P. (2010). “Disambiguating the Functions of Conversational Sounds with Prosody, The Case of Yeah”. Katika *Interspeech*. 4:1-11.
- Hoek, J. (2013). “Yeah no, I agre? T he Interpretation of Yes and No in Dutch”. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nijmegen.
- Hogeweg, L., de Hoop, H., Ramachers, S., der Slik, F., na Wottrich, V. (2016). The L2-acquisition of the German Particles *doch*, Katika *IRAL*, DOI 10.1515/iral-2016-9981.
- Jefferson, G. (1985). “Notes on a Systematic Development of the Acknowledgement Tokens “yeah” and “mm hm””. Katika *Paper in Linguistics*. 17:197-216.
- Jefferson, G. (1985). “Notes on a Systematic Development of the Acknowledgement Tokens “yeah” and “mm hm””. *Paper in Linguistics*. 17:197-216.
- Johnson, M. (1972). “Canadian Eh” katika *Ohio State University Working papers in Linguistics*. 21:153-160.
- Lenk, U. (1998). “Discourse Markers and Global Coherence in Conversations”. Katika *Journal of Pragmatics*. 30:245-257.
- Li, Wang. (2015). “Teaching in the Use of Pragmatic Markers for Chinese EFL Learners”. Katika *Universal Journal of Educational Research*. 3 (11) :822-829.
- Nasir, S, H. (2017). “The Interpretation of Discourse Markers *ya* ‘yes’ and *nggak* ‘no’ in Indonesia”. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Radboud.
- O’Neal, G. C. (2013). “Teological and Dolichological Discourse Marking in Oral American Media: The Discourse Markers “So” and “Ok”. Tasnifu ya Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha London.
- Psathas, G., na T. Anderson. (1993). “The Practices of Transcription in Conversation Analysis” Katika *Semiotica*. 78 (1/2): 75-99.
- Redeker, G. (1991). “Review Article: Linguistic Markers of Discourse Structure”. Katika *Linguistics*. 29:1139-1172.
- Sacks, H., E. A., Schegloff na G. Jefferson. (1992). *Lectures on Conversation*. Oxford: Basil Blackwell.
- Schegloff, E. A. (1987). “Recycled Turn Beginnings: a Precise Repair Mechanism in Conversation. *American Journal of Sociology*. 97(5):1295-1345.

- _____(1992). "Repair After a Next Turn: The Last Structurally Provided Defense of Intersubjectivity in Conversation". *American Journal of Sociology*. 97(5):1295-1345.
- Schiffrin, D. (1987). *Discourse Markers*. Cambridge: CUP.
- Stede, M. (2000). Discourse Particles and Discourse Functions. *Katika Machine Translation*. 15: 125-147.
- Yang, S. (2011). Investigating Discourse Markers in Pedagogical Settings: A literature Review. *Katika ARECLS*. 8:95-108.
- Yilmaz, E. (2002). 'A practical Analysis of Turkish Discourse Markers: yan, iste and sey'. *Tasinifu ya Uzamivu (hajachapishwa)*. Middle East Technical University.
- Zarei, F. (2013). "Discourse markers in English" *katika International Research Journal of Applied and Basic Sciences*. Toleo 4(1):107-117).

Kiambatisho

Katika makala haya tumetumia alama mbalimbali zilizopendekezwa na Psathas na Anderson (1993) kama ifuatavyo:

ALAMA	MAANA
Namba 1- 101	Tamko la mzungumzaji mmoja au zamu tofauti za kuzungumza.
A, B, C	Kuwakilisha Majina ya wazungumzaji.
Herufi kubwa katika silabi au neno (Mfano, CHENJI)	Maneno yaliyosemwa kwa kuongezeka kwa sauti kuashiria msisistizo.
(())	Kufafanua matendo yanayofanywa na washiriki wa mazungumzo.
=	Mfululizo wa uzungumzaji; mzungumzaji wa pili ameanza kuzungumza mara tu baada ya mzungumzaji wa kwanza kumaliza au mzungumzaji huyohuyo ameongea jambo moja na kisha akaongea jambo jingine bila kupumzika.
Namba zilizowekwa katika mabano kwa mfano (0.5).	Muda wa ukimya.
[[]]	Mazungumzo yanayotokea kwa wakati mmoja (wazungumzaji wawili au zaidi wanaanza kuzungumza kwa wakati mmoja.
[]	mwingiliano katika mazungumzo (mzungumzaji mmoja anaingilia mazungumzo ya mzungumzaji mwingine.
:	Kiwango cha urefushaji wa silab. Semi koloni zitaongezeka au kupungua kutegemea na kiwango cha urefushaji wa silabi husika.
—	Mstari unaowekwa chini ya neno au silabi umetumika kuashiria mkazo (mfano njoo <u>hapa</u>).
°	Imetumika kuashiria sauti inayotamwa kwa kubembeleza au kwa upole.
,	Kiimbo cha kuendelea.
?	Kiimbo cha swali.
!	Kiimbo cha mshangao
...	Baadhi ya mazungumzo yameondolewa.